

## **MFUMO WA UTEKELEZAJI WA MASUALA YA MAZINGIRA NA JAMII KATIKA MRADI WA KUBORESHA UPATIKANAJI NA UTOAJI WA HODUMA BORA ZA KIMAHAKAMA ZANZIBAR (Z-JUMP)**

Banki ya Dunia inashirikianai na Mahakama ya Zanzibar katika kutekeleza mradi wake wa kuboresha huduma za Mahakama. Lengo la mradi huu ni kuimarisha na kuboresha Mahakama na Usimamizi wa Utumishi wa Umma kwa ajili ya kuboresha upatikanaji na ubora wa utoaji huduma Zanzibar. Mradi huu unatekelezwa kwa kuzingitia mfumo bora wa usimamizi wa maswala ya mazingira na jamii.

### **LENGO LA MFUMO WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA JAMII**

Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMF) Umeandaliwa kwa ajili ya kuhakikisha utekelezaji wa masuala ya mazinira na jamii kwa kiwango cha kimataifa kwa kuzingatia viwango vya Bank ya Dunia katika ufadhili wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na mradi wa uboreshaji wa upatikanaji na utoaji wa huduma za kimahakama Zanzibar.

### **SHUGHULI ZITAKAZOFANYIKA WAKATI WA UTEKELEZAJI WA MRADI.**

Shughuli kuu za Mradi ni pamoja na ujenzi wa mahakama za kisasa ( Smart Court) , ukarabati wa majengo ya Mahakama katika maeneo yaliyochaguliwa, kujenga uwezo wa kufanya kazi ya matumizi ya ADR na kuendeleza Mahakama ya haki za kijinsia katikavisiwa vya Unguja na Pemba. Mfumo huu wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMF) umeandaliwa kutambua athari za kimazingira na kijamii za Mradi zilizopendekezwa na kuanzisha hatua zinazofaa za kukabiliana na athari kwa mujibu wa sheria/kanuni za Mazingira ya Zanzibar na Viwango vya Mazingira na Jamii vya Benki ya Dunia (ESSs) kutumika kwa mradi huo. Shughuli za mradi ambazo zinatarajiwa kuwa na athari kwa mazingira ni pamoja na shughuli za ujenzi.

Athari zinazohusiana na kazi za kiraia wakati wa ujenzi wa mahakama ya “smart” ni pamoja na uhamiaji wa watu kutoka maeneo mbalimbali kurundikana katika eneo la mradi, kuondolewa kwa mimea, kelele, vumbi, uzalishaji wa taka, hatari za afya na usalama wa kazi, unyanyasaji, ukatili na ubaguzi wa kijinsia, ajira kwa watoto na athari katika afya ya jamii kama vile kuchochea maambukizi ya magojwa ikiwemo Ukimwi,Kifua kikuu, na magaojwa mengine mbali mbali ya kuambukiza.

Athari zinazohusiana na kuboresha kwa Mahakama kidigitali ,uwepo wao ni pamoja na uzalishaji wa taka za kielektroniki.

### **NJIA ZA KUKABILIANA NA KUPUNGUAZU ATHARI ZA MAZINGIRA NA JAMII KATIKA MRADI HUU.**

Ili kukabiliana na kupunguza athari mbalimbali za Mazingira na Jamii ,Tathmini malimbali zilifanyika na mipango kwa ajili ya utekelezaji imeandaliwa ili kuhakikisha mradi unatekelezwa

bila kuwa na matokeo hasi kwa jamii .Mipango iliyoandaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa masuala ya Mazingira na jamii ni pamoja na Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (Environmental and Social Management Framework (ESMF), Mpango wa kushirikisha wadau mbalimbali katika mradi (Stakeholders Engagement Plan(SEP), Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko ( Grievance Redress Mechanism), Mpango wa wa utayari wa kutekeleza masuala ya Mazingira na Jamii (Environmental and Social Commitment Plan (ESCP) na Mpango wa usimamizi wa wafanyakazi wakati wa utekelezaji wa mradi (Labour Management Plan)

Nyaraka zote zilizoandaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi zimebekwe katika tovuti ya Mahakama kwa ajili ya wananchi na wadau mbalimbali kuzisoma na kupata taarifa zaidi kuhusu utekelezaji wa mradi huu. Zinapatiakana katika tovuti ya mahakama ambayo ni :  
<https://judiciaryzanzibar.go.tz/web/zijump>